# TAARIFA YA MHE. ENG. EVARIST NDIKILO, MKUU WA MKOA WA PWANI KWA MHE. KASSIM M. MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA ZIARA YAKE MKOANI PWANI TAREHE 23 MEI 2017

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Awali ya yote tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai uliotuwezesha kukutana hapa leo tukiwa salama.

Pili, sisi Viongozi na Wananchi wa Mkoa wa Pwani kwa moyo wa dhati kabisa kwa mara nyingine tunakukaribisha wewe na msafara wako Mkoani Pwani kuja kuona juhudi zinazofanywa na wananchi na wawekezaji mbalimbali za kujenga viwanda ikiwa ni utekelezaji wa Kauli Mbiu ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Ujenzi wa Viwanda.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Hali ya Ulinzi na Ulinzi na Usalama Mkoani Pwani kwa jumla ni shwari na wananchi wanaendelea na shughuli zao za uzalishaji mali. Hata hivyo, yapo matukio ya kiuhalifu ya mauaji ya viongozi wa ngazi za Vitongoji na Vijiji katika Wilaya za Rufiji, Kibiti na Mkuranga. Pia, yapo matukio madogo madogo yanayojitokeza hapa na pale, kwa mfano, ujambazi wa kutumia silaha, migogoro ya wakulima na wafugaji na uhalifu mwingine. Matukio yote haya yanashughulikiwa na vyombo vyetu vya dola kadri yanavyojitokeza

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Zoezi la Ujenzi wa viwanda Mkoani Pwani linaendelea vizuri sana. Ndani ya kipindi kifupi tangu ulipofanya ziara yako miezi ya Julai na Septemba mwaka jana, viwanda saba (7) vimekamilika na kuanza uzalishaji. Viwanda hivyo ni:-

(i) Goodwill Ceramic (T) Limited kilichopo Mkiu Wilayani Mkuranga kinachotengeneza marumaru (tiles).

(ii) Kiwanda cha Kiluwa Steel Group of Company kinachotengeneza nondo za aina mbalimbali.

(iii) Kiwanda cha Global Packaging kilichopo eneo la Mnarani-Kibaha kwa ajili ya kutengeneza vifungashio.

(iv) Kiwanda cha Elven Agriculture Company Limited kilichopo Mapinga Bagamoyo kwa ajili ya kukausha matunda.

(v) Kiwanda cha East Africa Infrastructure Engineering Limited kilichopo Fukayosi Bagamoyo kwa ajili ya kutengeneza nguzo za zege za umeme na simu.

(vi) Kiwanda cha Vegeta Podravka Ltd kilichopo Bagamoyo kwa ajili ya kutengeneza viungo vya kuongeza radha ya chakula

(vii) Kiwanda cha kuunganisha matrekta cha TAMCO (TAMCO Tractor Assembling Plant) chini ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC ambacho umepata fursa ya kukitembelea hii leo.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Tunawapongeza Wizara na NDC kwa kuendeleza juhudi za Mkoa za kuvutia uwekezaji wa Viwanda. Kiwanda hiki ulichokitembelea leo ni cha aina yake nchini katika uundaji wa zana za kilimo. Ni

kiwanda muhimu na kimechangia zaidi kuuweka Mkoa wa Pwani katika ramani ya uwekezaji. Hata hivyo, tunaiomba Wizara na NDC kutimiza ahadi yao ya kulisawazisha eneo lililobaki lenye ukubwa wa karibu ekari 230 na kuliwekea miundombinu stahiki ili kuvutia wawekezaji zaidi na hivyo kuboresha kitovu cha Mji wa Kibaha.

Aidha, tunatoa wito maalum kwa Shirika la Elimu Kibaha wanaomiliki eneo la upande mwingine wa barabara, ambalo kwa sehemu kubwa ni vichaka kuiga mfano wa NDC kwa kuliandaa eneo ili kuvutia wawekezaji kujenga viwanda ili tuboreshe Mji wetu na kutoa ajira kwa wana-Pwani na Watanzania kwa jumla.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Licha ya Viwanda vinavyofanya kazi, tuna viwanda vingine, vikubwa na vya kati vinavyoendelea na hatua mbalimbali za ujenzi kwa kasi inayoridhisha na vinatarajia kuanza uzalishaji mwaka huu au mapema mwakani. Baadhi ya Viwanda hivyo tukitaja vichache ni kama ifuatavyo:-

(i) Kiwanda cha Sayona kilichopo Mboga Chalinze, kwa ajili ya kutengeneza juisi za matunda ya aina mbalimbali.

(ii) Kiwanda cha Twyford Ceramics (T) Company Ltd kilichopo Pingo Chalinze kwa kwa ajili ya kutengeneza marumaru (tiles)

(iii) Kiwanda cha KEDS kilichopo Kibaha kwa ajili ya kutengeneza sabuni.

(iv) Kiwanda cha Kamal Oil Refinery cha Vilainishi kipo Kerege.

(v) Kiwanda cha Kamal Agro cha Nafaka kipo Kerege.

(vi) Kiwanda cha PHISS Turnery cha bidhaa za ngozi kipo Zinga.

(vii) Kiwanda cha INOVA Company Ltd cha Betri kilichopo Zinga.

(viii) Kiwanda cha Tube Limited cha Vifaa vya Ujenzi kilichopo Zinga.

(ix) Kiwanda cha African Dragon Enterprises cha kutengeneza mabati kipo Zinga.

(x) Kiwanda cha Hauteng Metallurgical Co. Ltd cha kutengeneza Nondo.

(xi) Kiwanda cha Zinga Pharmaceuticals Company Ltd, kitakachotengeneza madawa ya aina mbalimbali ya binadamu. Mchakato wa ujenzi wa kiwanda hiki upo tayari na wataalam kutoka Ujerumani wapo nchini kwa ajili ya ujenzi huo.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Pamoja na jitihada hizi zinazoendelea, sambamba na Halmashauri zetu kuendelea kutenga maeneo zaidi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda, kumekuwa na changamoto kuu tatu (3) ambazo kama hazitafanyiwa kazi haraka zinaweza kupunguza kasi ya ujenzi wa viwanda, kama ifuatavyo:-

(i) Changamoto ya nishati ya umeme wa uhakika. Kutokana na ongezeko la matumizi ya umeme viwandani na majumbani, umeme umekuwa unakatikatika sana kwa sababu ya kuzidiwa kwa vituo vya kupozea umeme vya Mlandizi na Chalize. Aidha, viwanda vya Mkuranga vinategemea umeme kutoka kituo cha Kipawa ambapo ni mbali sana. Kutokana na

changamoto hii tumefanya mazungumzo na Wizara ya Nishati na Madini na TANESCO Kanda na Mkoa kuhusu kuboresha huduma hii. Mapendekezo ya Mkoa ni kuwa na vituo vya kupozea umeme kulingana na ramani ya uwekezaji kwa maana na Bagamoyo Loop, Kibaha – Chalinze Loop, Kisarawe Loop na Mkuranga, Kibiti - Rufiji Loop. Wizara na TANESCO wanalifanyia kazi suala hili. Tunaomba msukumo wa Serikali Kuu ili suala hili liende haraka.

(ii) Changamoto ya Nishati ya Gesi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Wawekezaji karibu wote wanaofika Mkoani kwetu wanauliza "Je gesi ipo karibu na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kujenga viwanda?". Maeneo ya Kisarawe, Kibaha, Chalinze na Bagamoyo yanaweza kukosa uwekezaji kwa sababu ya kuwa mbali na bomba la gesi. Suala hili linahitaji mkakati wa kitaifa wa jinsi ya kuisambaza nishati hii kwenda kwenye maeneo yanayokusudiwa kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda.

(iii) Changamoto ya Maji ya uhakika. Changamoto hii ni kubwa sana hasa kwa Wilaya za Kisarawe, Mkuranga, Kibiti, Rufiji na Bagamoyo (hasa Halmashauri ya Chalinze kutokana na kutokuwa na vyanzo vya uhakika vya maji. Mapendekezo ya Mkoa ni kuona bomba la maji la Ruvu Juu linakuwa na tawi eneo la Mlandizi kuelekea maeneo ya Viwanda ya Kikongo na Mihugwe linalomilikiwa Kiluwa Group. Aidha, kuwepo na tawi eneo la Kiluvya kulisha eneo la Viwanda la Visegese hadi

Kisarawe mjini kwa ajili ya viwanda na matumizi ya majumbani. Tunakusudia kufanya majadiliano na DAWASCO ili kuona namna bora ya kutekeleza suala hili. Tunaomba pia msukumo wa Serikali Kuu ili suala hili lipewe kipaumbele.

***Mheshimiwa Waziri Mkuu,***

Kama nilivyosema awali, Pwani tunajenga viwanda. Tutaendelea kuvutia wawekezaji zaidi ili waendelee kujenga viwanda zaidi. Tunaishukuru Serikali kwa kuendelea kutuunga mkono katika jitihada hizi. Tunamshukuru sana Mhe. Rais kwa kuzindua na kuweka jiwe la msingi kwenye viwanda vya Bakhresa na Goodwill vyote vya Mkuranga. Aidha, tunakushukuru wewe binafsi kwa kazi kubwa unayoifanya ya kufuatilia kwa karibu maendeleo ya viwanda Mkoani Pwani. Tunamshukuru Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji Mhe. Charles Mwijage kwa kuwa karibu wakati wote na Mkoa wa Pwani katika jitihada hizi. Tunaahidi kuendeleza jitihada hizi ili azma ya kuwa na uchumi wa kati kupitia viwanda inafikiwa.

***Asanteni sana kwa kunisikiliza na Karibuni sana Mkoani Pwani.***

Eng. Evarist Ndikilo
**MKUU WA MKOA**